**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA, KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza vyema nchi yetu pamoja na watu wake. Hekima na busara kubwa anazoendelea kuzichukuwa Mheshimiwa Rais zinasaidia sana katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu. Sote ni mashahidi kwamba, kuimarika kwa amani na utulivu nchini, ndio chachu ya maendeleo hayo. Aidha, pongezi pia ziwaendee Makamo wa kwanza wa raisi Mheshimiwa Othman Masoud Othman pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdallah kwa namna wanavyoshirikiana vyema na Mheshimiwa Rais katika kutekeleza

majukumu hayo mazito ya Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, nachukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wa baraza, Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma pamoja na Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo** kwa jitihada zenu na namna mnavyoliongoza baraza hili tukufu kwa weledi na uadilifu wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Mheshimiwa Omar Said Shaaban, Katibu Mkuu ndugu Ali Khamis Juma, Afisa Mdhamin ndugu Ali Suleiman Abeid, Wakuirugenzi pamoja na watendaji wote kwa jitihada kubwa wanazoendelea kuzichukuwa katika kuiletea nchi yetu maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Wajumbe hawa walionekana kuwa makini na walitumia taaluma na uwezo wao katika kutoa michango yenye tija wakati wa uwasilishwaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii. Michango ambayo ililenga katika kuhakikisha kuwa, sekta ya biashara na viwanda zinakuwa na kuinaimarika nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena niwatambuekwa majina wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Yussuf Hassan Idd | Mwenyekiti |
| 2.Mhe. Aza Januar Joseph | Makamo Mwenyekiti |

| | |
|---|---|
| 3.Mhe. Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 4.Mhe.Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5.Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 6.Mhe. Said Saleh Salim | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati hii inafanya kazi zake kwa karibu sana na makatibu wawili ambao ni:

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Abuubakar Mahmoud Idd | Katibu |
| 2. Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kila mwaka wa fedha, kama Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ilivyoelekeza. Katika kulitekeleza jukumu hili, Kamati ilikutana na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda siku ya Jumanne ya tarehe 02/05/2023 kwa lengo la kupitia, kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshmiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepangiwa kutekeleza Programu Kuu tatu (3) kama ifuatavyo:

i) Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara;

ii) Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali;

iii) Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara;

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii imebeba nguvu kazi ya Wizara nzima, ikiwemo Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuipangia Matumizi ya jumla ya shilingi **bilioni 4.053** kwa mwaka wa fedha ujao, 2023/2024 fedha ambayo imeongezeka ukilinganisha na Makadirio kwa mwaka wa fedha uliopita 2022/2023, ambapo ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi **bilioni 2.977.** Kamati inaamini kwamba, ongezeko hili la fedha litasaidia sana kuongeza kasi ya utekelezaji wa majukumu kwa mwaka huu wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umuhimu wa shughuli zilizolengwa kutekelezwa na Programu hii kwa mwaka huu wa fedha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuingiza fedha hizo kwa wakati ili waweze kufanikisha majukumu yao kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Utekelezaji mzuri wa majukumu ya Wizara utafanikiwa endapo wafanyakazi watajengewa mazingira mazuri yatakayoweza kujenga mori katika utekelezaji wa majukiumu yao ya kila siku. Katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za Wizara, Kamati imebaini changamoto kubwa ya upatikanaji wa ofisi za kudumu kwa Wizara hii, jambo linalorudisha nyuma kasi ya utendaji na ufanisi kwa taasisi zetu. Kamati imeshuhudia ufinyu wa ofisi kwa taasisi zilizomo katika Wizara hii, pamoja na hamahama kwa taasisi kutoka sehemu moja kwenda nyengine, hali inayorudisha nyuma juhudi za

watendaji katika kutekeleza majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuharakisha mchakato wa ujenzi wa ofisi za Serikali ili Wizara hii nayo iweze kupata ofisi za kudumu na kuepusha hamahama iliyopo hivi sasa.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**Mheshimiwa Spika,**

Utekelezaji wa Programu hii unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda ikilenga kuimarisha sekta ya viwanda pamoja na kuwanyanyua wajasiriamali katika kuendeleza biashara zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2023/2024, imejipangia malengo mazuri katika kufikia uchumi wa viwanda utakaotuwezesha kujitegemea kwa asilimia kubwa katika mipango, makusanyo na matumizi ya fedha zetu wenyewe. Baada ya kupitia bajeti hii, Kamati imebaini kwamba Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inatarajia kuendelea kuyaimarisha maeneo ya viwaanda ya Dunga na Chamanangwe, kwa kuyazunguushia uzio, kujenga majengo ya viwanda, kukamilisha miundombinu ya umeme pamoja na kutengeneza barabara za ndani kwa upande wa Dunga. Aidha, katika kuhakikisha kwamba, Zanzibar inakuwa na neo lake la kudumu litakalotumika katika maonesho ya kibishara, Wizara imepanga kujenga ukuta na majengo ya maonesho ikiwa ni pamoja na ujenzi wa magazebo, mantenti madogo na samani.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezo zake za dhati kwa Wizara ya Biashara kupitia Idara yake ya Maendeleo ya Viwanda, kwa mipango yake mizuri yenye lengo la kubadilisha taswira ya nchi yetu na kuifanya iwe ni nchi ya viwanda. Lakini

ni ukweli usiopingika ya kwamba, endapo fedha iliyopangwa kutumika kwa utekelezaji wa shughuli hizi hazikupatikana, mategemeo ya Wizara juu ya hili hayatafikiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango, kuwaingizia fedha iliyopangwa kwa wakati. Kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024, Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi **bilioni 2,404**.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hali hiyo, Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa juhudi inazoendelea nazo katika kuhakikisha kuwa, sekta ya viwanda inapiga hatua nchini. Maendeleo mazuri ya ujenzi wa kiwanda cha mwani huko Chamanangwe kisiwani Pemba na malengo ya kujenga kiwanda kipya cha mwani aina ya Ulva, kisiwani Unguja katika maeneo ya uwekezaji Dunga, kwa kushirikiana na wawekezaji kwa njia ya ubia ni hatua za kupigiwa mfano. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara, kuharakisha mchakato wa kuwapatia wawekezaji hao eneo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho, ili nchi yetu izidi kupiga hatua kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, kutokana na umuhimu wa sekta hii ya viwanda nchini, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa zao la mwani kwa lengo la kuongeza kasi ya uzalishaji wake, ili viwanda hivi vitakapomalizika viweze kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali ijikite ipasavyo katika kuiendeleza sekta hii ya **viwanda na biashara**. Kamati inaamini kwamba endapo Serikali itaandaa mazingira mazuri ya kuzikuza kikamilifu sekta hizi, uchumi wa taifa letu utaweza kukua kwa kasi na itasaidia sana katika kupunguza makali ya muelekeo wa anguko la uchumi kwa taifa letu.

## PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inalenga kuimarisha nafasi ya Zanzibar Kupitia biashara na usafirishaji wa bidhaa kwa masoko ya Kitaifa na Kimataifa. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka ujao wa fedha **2023/2024,** ya kujenga vituo jumuishi kwa ajili ya urasimishaji Biashara (MKURABITA) katika maeneo ya Bopwe kwa upande wa Pemba na Tunguu kwa Unguja. Vituo hivi ni muhimu sana kwa wafanya biashara waliopo nchini katika kuwajengea uwelewa kuhusiana na umuhimu wa kurasimisha biashara zao. Aidha vituo vitaweza kuwatambulisha wafanyabiashara hao na kuweza kupata fursa ya kurasimisha biashara zao kutoka mfumo usio rasmi.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuyafanikisha malengo hayo, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuwaingizia fedha za kutosha ili malengo ya kujenga vituo jumuishi kwa ajili ya Urasimishaji wa biashara yaweze kutekelezwa kwa wakati na nchi yetu viweze kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo na tuweze kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknologia yanayoendelea kukuwa duniani hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inaipongeza kwa dhati Taasisi ya Viwango (ZBS) kwa jinsi inavyojitoa katika utekelezaji wa majukumu yake, ambapo kwa kupitia vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imelenga kukamilisha kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto katika eneo liliopo mkabala na Ofisi ya ZBS Maruhubi, ambacho kitakuwa na uwezo wa kukagua vyombo vya moto 300 kwa siku. Kukamilika kwa kituo hiki kutasaidia sana kuondosha usumbufu uliopo hivi sasa katika ukaguzi wa vyombo hivyo. Kwa dhati kabisa, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Taasisi ya Viwango Zanzibar, kwa kuukamilisha ujenzi wa kituo hiki katika

wakati muafaka na kutoa ushauri kwa taasisi hii kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa kasi zaidi na nchi yetu iweze kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**,

Aidha, Kamati inaendelea kutoa pongezi zake kwa Taasisi ya Viwango Zanzibar, kwa kuendelea kuihami jamii yetu juu ya matumizi sahihi ya viwango kwa bidhaa zinazoingia nchini. Ujenzi wa Maabara nne ndani ya Taasisi hii, utasaidia sana katika kuboresha matumizi hayo. Kamati inaishauri taasisi hii kuendelea kutoa elimu kwa jamii, wadau pamoja na wajasiriamali katika kuona umuhimu wa kuzipima bidhaa zao. Aidha, Taasisi hii ni vyema ikazitunza Maabara hizi ikiwa ni pamoja na vifaa vyote vilivyonunuliwa kwa ajili ya kuziendesha maabara hizi, ambavyo vimenunuliwa kwa gharama kubwa.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

**Mheshimiwa Spika**,

Jukumu la msingi la Shirika hili ni kuuza na kununua karafuu na mazao mengine ya viungo nchini. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imelenga kuimarisha vitega uchumi vya Shirika ikiwa ni pamoja na kukamilisha Ujenzi wa Maghala ya kuhifadhia Karafuu Madungu, Ujenzi wa nyumba – Malindi kwa ajili ya kuikodosha. Aidha, Wizara imelenga kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mimea unaotarajiwa kuongezeka kutoka tani 22 hadi tani 34.1 kwa mwaka huu wa fedha 23/24.

**Mheshimiwa Spika**,

Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupitia Shirika hili, kuwa wabunifu katika kutekeleza majukumu yake. Shirika lijikite zaidi katika kutafuta vitega uchumu vingi zaidi vitakavyosaidia kulikuza Shirika. Aidha Shirika lijiwekeze zaidi katika taasisi za kifedha ili kutanua wigo na kuona namna ya kutafuta masoko ya nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini. Pamoja na hali hii, Kamati inalishauri Shirika

la Biashara la Taifa (ZSTC) kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kufanya utafiti wa kina juu ya tatizo la kukauka kwa mikarafuu lililojitokeza kaskazini mwa kisiwa cha Unguja hivi karibuni, tatizo hili endapo litachiwa liendelee linaweza kuathiri kilimo cha Mikarafuu nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha kuwa mafanikio makubwa yanapatika ndani ya Shirika hili, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, ihakikishe inapanga mikakati ya kuliboresha Shirika liweze kujiendesha kibiashara. Shirika lazima liwe na ubunifu katika kuhakikisha kuwa, Shirika linarudi katika hadhi yake na liweze kufikia hatua ya kutoa gawio serikalini.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kuhusiana na bajeti ya Wizara hii ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.  Niwashukuru pia wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa. Sasa niwaombe wajumbe wako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kuyatekeleza yale waliyojipangia kwa mwaka huu wa fedha unaokuja.

**Mheshimiwa Spika**,

Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Kamati yangu ya Kilimo, Biashara na Utalii naunga mkono hoja kwa 100%.

**Mheshimiwa Spika**,

Baada ya maelezo hayo, **naomba kuwasilisha**.

**Ahsante sana,**

…………………………………………

**Yussuf Hassan Idd,**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**<u>Zanzibar</u>.**